

## Haki katika Misitu Tanzania

Haki katika Misitu Tanzania ni mradi unaoshughulika na kuimarisha utawala bora na kuboresha uwajibikaji katika sekta ya misitu Tanzania. Mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano wa Shirika la kuhifadhi misitu ya asili Tanzania (TFCG) na Shirika la Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) na unafadhiliwa na Mfuko wa AcT. Mradi utatekelezwa kwa muda wa miaka mitatu kuanzia mwaka 2011 mpaka 2013

### Lengo kuu la Mradi

Huduma zinazotokana na mfumo ikolojia wa misitu zinahifadhiwa kwa manufaa ya jamii na taifa.

### Malengo mengine ya mradi

- Kuimarika kwa utawala bora katika sekta ya msitu
- Watanzania kufaidika na huduma zitolewazo na mfumoikolojia wa misitu

### Sehemu Mradi unapotekelezwa

Mradi unatekelezwa katika kanda sita za jamii zinazoishi kando kando ya misitu ya asili na zinazoshiriki katika usimamizi shirikishi jamii wa misitu. Kanda hizo ni:

- Kaskazini katika mikoa ya Tanga, Moshi na Arusha
- Kusini katika mikoa ya Lindi, Kilwa na Mtwara
- Mashariki katika mikoa ya Mororgoro, Pwani na Dar es Salaam
- Nyanda za juu kusini mkoa wa Iringa
- Kanda ya Kati katika mkoa wa Manyara, Dodoma na Singida
- Kanda ya Magharibi katika mkoa wa Kigoma.

Kwa mwaka wa 2011, mradi utatekeleza shughuli zake kwenye kanda za kaskazini, kusini na mashariki, na kanda nyingine zitafikiwa kuanzia mwaka 2012 na 2013.

## Utekelezaji wa Mradi

Ili kufikia malengo yaliyokusudiwa, Mradi umejiwekea mikakati minne ifuatayo:-

### Mkakati wa Kwanza: Ufuatiliaji utawala wa misitu na hali ya misitu

Mradi utaanzisha mfumo wa ufuatiliaji utawala wa misitu na hali ya misitu katika jamii zinazotekeleza mipango ya uhifadhi wa misitu pamoja na kufahamu hali halisi ya misitu hiyo. Matokeo ya mfumo huo yatasaidia jamii kuibua matatizo mbalimbali ya kiutawala na hivyo kuchochea mabadiliko katika sekta ya misitu.

Shughuli zitakazofanyika katika mkakati huu:

1. Kuanzisha na kutekeleza mfumo wa ufuatiliaji wa utawala wa misitu katika ngazi ya jamii na Serikali.
2. Kutoa mafunzo mbalimbali yanayohusu uongozi, usimamizi wa misitu nakadhalika ili kuziwezesha jamii kujifunza pamoja katika usimamizi shirikishi jamii.
3. Kufanya ufuatiliaji wa hali ya misitu.

### Mkakati wa pili: Kuhamasisha utekelezaji wa sheria za misitu

Mkakati huu una lengo la kuhimiza Serikali kuu na Serikali za mitaa kuwa makini zaidi katika kupambana na uhalifu wa misitu pamoja na kuzijengea uwezo jamii kuchukua hatua dhidi ya mapungufu ya Serikali katika utawala katika sekta ya misitu.

Shughuli zitakazofanyika katika mkakati huu;

1. Kutambua na kuripoti masuala yanayohusu utawala wa misitu kwa njia ya mtandao maalumu wa simu wa kupokea ripoti za jamii zinazohusu uhalifu unaofanywa katika misitu kwa njia ya kuimarisha mitandao ya MJUMITA.
2. Kufuatilia kesi za uhalifu wa misitu kwa kushirikiana na mamlaka husika kama vile Polisi, Mahakama, Serikali za vijiji n.k
3. Kuziwezesha jamii kukabiliana na mapungufu ya utawala katika misitu
4. Kuratibu mfumo wa tovuti unaohifadhi taarifa za matukio ya uhalifu yanayoripotiwa na wanajamii na mwendelezo wa ufuatiliaji wa taarifa hizo. Tovuti hii itakuwa wazi kwa kila mtu

### Mkakati wa tatu: Tafiti, Chambuzi na Mawasiliano

Mradi utafanya tafiti na chambuzi mbalimbali kubaini vikwazo katika kuboresha utawala na uhifadhi wa misitu.





Shughuli zitakazofanyika katika mkakati huu:

1. Kufanya tafiti zinazohusu utawala wa misitu.
2. Kupashana habari kwa kutumia vyombo vya habari, kuchapisha makala mbalimbali na mikutano kuhusu masuala yanayohusu utawala katika misitu.

## Mkakati wa nne: Matumizi ya viwango vya kimataifa

Mradi utafanya kazi ya kuchochea matumizi ya viwango vya kimataifa, hii itajumuisha  Mpango wa kupunguza hewa ya ukaa kutokana na ukataji wa miti ovyo na uharibifu wa misitu (MKUHUMI) na matumizi ya taratibu za uvunaji, usafirishaji na biashara ya mazao ya misitu kimataifa.

Shughuli zitakazofanyika katika mkakati huu:

1. Mapitio ya njia bora za usimamizi wa misitu hasa katika uhusiano wa MKUHUMI na uvunaji mbao.
2. Kuhamasisha sekta binafsi ili kutumia njia bora za usimamizi wa misitu zenye mahusiano na MKUHUMI na uvunaji mbao.
3. Kuendeleza usambazaji wa taarifa za taratibu za uvunaji,usafirishaji na biashara ya mbao kwa jamii

## MJUMITA

Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) ni Muungano wa vikundi vya jamii zinazoishi kando kando ya misitu ya asili ambazo zinashiriki katika usimamizi wa misitu Tanzania. MJUMITA inavisaidia vikundi hivi kuwa na nguvu ya pamoja juu ya masuala ya usimamizi misitu, utetezi kuhusu sera madhubuti za misitu pamoja na upashanaji habari.

Kwa mawasiliano andika
S.L.P 21522, Dar es Salaam
Simu: +255 22 2669007
Barua pepe:rnjaidi@gmail.com
Tovuti: www.mjumita.org

## Shirika la Kuhifadhi misitu ya asili Tanzania (TFCG)

Mipango ya TFCG ni kuhifadhi na kurejesha misitu yenye bioanuwai muhimu kimataifa kwa manufaa ya kizazi kilichopo na kijacho. TFCG imefanikiwa kutoa mbinu mbalimbali na ufumbuzi juu ya changamoto zinazoikabili sekta ya misitu Tanzania pamoja na watu wanaoitegemea.

Kwa mawasiliano andika
S.L.P 23410, Dar es Salaam
Simu: +255 22 2669007
Barua pepe: tfcg@tfcg.or.tz
Tovuti: www.tfcg.org

## Kwa mawasiliano ya kanda piga simu;

1. Kanda ya Kaskazini: 0788 434514
2. Kanda ya Mashariki: 0788 434517
3. Kand ya Kusini: 0788 434518

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

# Haki katika Misitu

## Kuboreshwa kwa utawala katika sekta ya misitu.

